



Toleo la FACT

FACT 96-03, Juni 1996 Tafsiri Januari 2006

Mwongozo mahsusi kuhusu miti yenye manufaa duniani

Mgunga - *Acacia mangium*: mti wenye manufaa katika nyanda za chini za nchi za hari

Acacia mangium Willd. Ni mojawapo ya miti inayokua kwa haraka na iliyo maarufu kule Asia na maeneo ya Pacific. Kutokana na uwezo wa kukua kwa haraka na kuhimili mchanga usio na rutuba, *A. mangium* ni mti ambao unatumiwa kwa wingi katika kuzalisha bidhaa za misitu pasipo kuathiri mazingira.

Ukuaji

Acacia mangium ni miongoni mwa miti ya jamii kubwa ya Leguminosae, na jamii ndogo ya Mimosoideae. Mti huu hukua kwa wepesi sana kiasi cha kufikia urefu wa 30m na kipenyo kinacho zidi 60cm (MacDicken na Brewbaker 1984). Maua yake yapo kwenye chana lililo na urefu wa hadi 10cm na maua meupe au eupe-manjano. Mau hayo yanaponawiri huonekana kama brashi ya chupa. Maua hayo yana manukato ya kuvutia. Majani ya rangi ya kijani iliyokolea yaweza kufikia urefu wa hadi 25cm na upana wa 10cm. Maganda ya mbegu ni mapana, yaliyopindika na upana wa 3-5mm huku yakifikia urefu wa 7-8cm.



Drawing by Gillian Rankin (courtesy of Queensland Herbarium, Indooroopilly, Queensland, Australia).

Mbegu zake ni za rangi ya hudhurungi au nyeusi inayong'aa na kati ya urefu wa 3-5mm na upana wa 2-3mm. Mbegu hukomaa baada ya miezi 6-7 ya kuota maua (Pinyopusarerk et al. 1993).

Acacia mangium ni mti ulio na nasaba za kizazi cha $2n=26$. Miti iliyoimarishwa kutoka kwa *A. auriculiformis* ni aina ya miti iliyo na matumaini makubwa katika kukuza misitu. Miti iliyoimarishwa ina uwezo wa kuhimili magonjwa na matatizo ya kuoza kuliko aina ya *A. mangium*, hata hivyo mti ulioimarishwa haufikii kina kirefu. Mti ulioimarishwa hukua imara na wima huku ukiweza kupunguza matawi kama ilivyo na aina ya *A. auriculiformis* (Ibrahim 1993).

Mazingira na maenezi

Acacia mangium ni mti uliotokea kule Australia, Indonesia na Papua New Guinea, lakini kwa hivi sasa umeenea hadi maeneo ya latitudo kuanzia 19° S hadi 24° N na longitudo kati ya 88° hadi 146° E. Acacia mangium ni aina ya mgunga unaoweza kufanya vyema katika nyanda za chini katika misitu ya mvua nyingi, mchanga wa siki usio shikilia maji (pH 4.5-6.5). Mwinuko ni kati ya 100m kutoka baharini, na juu zaidi kufikia 780m. Mti huu hupatikana katika maeneo ya unyevu, sehemu za nchi za hari zilizo na kipindi kifupi cha ukame na kiasi cha mvua kati ya 1446 na 2970mm kwa mwaka. Acacia mangium yaweza pia kukidhi kiwango cha mvua hadi 1000mm. Viwango vya joto kwa mwezi ni kati ya $13-21^{\circ}\text{C}$ kwa kiwango cha chini na $25-32^{\circ}\text{C}$ kwa kiwango cha juu. Licha ya kwamba mti huu ni wa rangi ya kijani mwaka mzima, *A. mangium* haitaweza kunawiri wakati wowote mwaka mzima. Ukuaji hupungua au kukoma iwapo kiwango cha mvua kitapungua au kiasi cha joto kushuka. Katika kipindi kirefu cha theluji, mti huu huangamia ($5-6^{\circ}\text{C}$).



<http://www.winrock.org>

Marejeleo yanayopendekezwa

Bray, R.A., Palmer, B., Ibrahim, T.M. (1997). Matokeo ya miti ya jamii ya vibweta-kunde katika sehemu nne za Indonesia na Australia. *Tropical Grasslands* 31(1):31-39.

Brook, R.M. (1993) Kupanda viazi vitamu katika utaratibu wa misitu kule Papua New Guinea. Makala ya miti ya Kuongeza Naitrojini 11:35-39.

Brook, R.M., Kanua, M.B., Woruba, M.G. (1992). Miti kwa matumizi ya kila aina kule Papua New Guinea: Matokeo ya awali. Makala ya miti ya Kuongeza Naitrojini 10:77-80.

Cole, T.G., Yost, R.S., Kablan, R., Olsen, T. (1996). Uwezo wa aina kumi na mbili ya *Acacia* kunawiri kwenye mchanga wa siki kule Hawaii. *Forest Ecology and Management* 80:175-86.

Dzowela, B.H. (1994) *Acacia angustissima* aina ya mti wa Amerika ya Kati uliofaulu. *Agroforestry Today*, 6 (3):13-14.

Orodha kamili yaweza kupatikana kutoka kwa tuvuti ya FACT Net

Makala yalitayarishwa na D. Preece & R. Brook, Kitivo cha Kilimo na Huduma za Misitu, Chuo Kikuu cha Wales, Bangor, North Wales, United Kingdom LL57 2UW
Kipepesi: 44 1248 354977
Barua-pepe: r.m.brook@bangor.ac.uk

Toleo la Forest, Farm, & Community Tree Network (FACT Net)
(Iliyokuwa Nitrogen Fixing Tree Association)

Winrock International

38 Winrock Drive

Morrilton, Arkansas 72110-9370, USA

Simu: 501-727-5435

Kipepesi: 501-727-5417

Barua-pepe: forestry@msmail.winrock.org

www.winrock.org/forestry/factnet.htm



<http://www.winrock.org>

Majulisho

Tafsiri na: PATRICK BUNYALI KAMOYANI
Barua-Pepe: pbkamoyani@lycos.co.uk au pbkamoyani@excite.com
Maragoli, Kenya

Toleo la Fact

www.winrock.org/forestry/factnet.htm